BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

**Kikao cha Kumi na Nane – Tarehe 27 Mei, 2025**

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

76. MHESHIMIWA CHUMU KOMBO KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Ili wafanyakazi wetu wafanye kazi zao vizuri, ni muhimu kuwa na vitendea kazi vya kutosha na kupatiwa maeneo bora ya kiutumishi ikiwa ni pamoja na majengo.

Je, Wizara yako ina mpango gani wa kuhakikisha watumishi wa umma wanapatiwa vitendea kazi vya kutosha ili kufanyakazi zao katika mazingira bora ya utulivu.

### Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

118. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Ni njia gani mbadala ambayo Serikali inaifikiria na kuipendekeza kwa wajasiriamali wanaojishughulisha na kuuza mkaa Mwanakwerekwe ili kuendeleza kampeni ya matumizi ya mitungi ya gesi.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

267. MHESHIMIWA BAHATI KHAMIS KOMBO (Jimbo la Chambani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka Mawakala wa Bima katika vijiji pamoja na mabango kama vile ya PBZ, CRDB na NMB.

**Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:**

184. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Ni mambo gani ya kujivunia kutokana na mageuzi makubwa yanayofanywa na Mhe. Rais katika sekta ya michezo.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

288. MHESHIMIWA HAJI SHAABAN WAZIRI (Jimbo la Uzini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Maendeleo ya teknolojia katika kilimo na umwagiliaji yamekuwa yakiendana na udhibiti wa athari za kimazingira, hasa kwa nchi ndogo za visiwa ikiwemo Zanzibar, kwa kuongeza ufanisi wa matumizi ya maji safi na maji taka.

Ni lini Wizara yako itaona haja ya kuzalisha wataalamu wa ndani kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ili kuondokana na upungufu wa wataalamu wa maji safi na maji taka.

**Wizara ya Afya:**

35. MHESHIMIWA DKT. MOHAMMED ALI SULEIMAN (Jimbo la Mtambwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kipindi cha nyuma Serikali ilisaidia kupitia wafadhili kuwa na utaratibu wa kutafuta gari binafsi katika shehia ili ziweze kuwasaidia wazazi wanaopaswa kufikishwa katika hospitali za Wilaya maarufu kama M-Mama ili kuweza kuokoa maisha ya mama na mtoto. Ni muda sasa huduma hii haipatikani hali inayopelekea shida kubwa kwa mama wajawazito katika baadhi ya shehia.

(a) Ni sababu gani zilizopelekea kuondolewa kwa huduma ya M-Mama.

(b) Ni ipi tathmini ya vifo vya mama na mtoto baada ya huduma hii kukosekana katika shehia.

(c) Ni upi mkakati wa Serikali katika kutatua tatizo hili ambalo linagharimu maisha ya mama wajawazito.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

225. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kiasi gani wanafunzi wataweza kupatiwa dhana ya mafunzo ya uhalisia ndani ya viwanda mbali mbali vilivyopo nchini.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

149. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Kiutafiti, kuna aina ngapi na zipi za mitindo ya ujenzi (Architectural designs) ndani ya Mji Mkongwe na kwa kiasi gani zinaenziwa.

150. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Milango ya Zanzibar maarufu kwa jina la 'Zanzibar Doors' imejijengea umaarufu mkubwa sana duniani kwa aina ya upekee wake.

Ni kwa kiasi gani Serikali inachukua jitihada za makusudi ku "brand" milango hii ili iendelee kuitangaza nchi yetu kiutalii na kiuchumi.

**II. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Afya:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa mwaka 2025/2026.

**Zanzibar,**
**27 Mei, 2025.**

**(Raya Issa Msellem)**
**KATIBU WA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR**